THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

121/1 **KISWAHILI 1**

(Kwa Watahiniwa Wasiokuwa Shuleni tu)

*Muda: Saa 3* *Jumatatu, 8 Februari 2010 asubuhi*

---

## MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina maswali **kumi na tatu (13)** katika sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **matano (5)** kwa kuchagua swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama **ishirini (20)**.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 5 zenye maandishi.

TATA PRINT 2010

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 20)

## HISTORIA YA KISWAHILI

1. "Kuiteua lahaja moja ili itumike kwa minajili ya kukisanifisha Kiswahili ilikuwa na kasoro zake." Jadili kasoro hizo.

2. "Usanifishaji wa lugha huipa lugha ulinganifu wa matumizi, maana na tahjia ya msamiati wa lugha husika." Jadili ukweli wa hoja hiyo.

3. Jadili muathiriano wa Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu.

## SEHEMU B (alama 20)

## SARUFI

4. Fafanua dhima tano (5) za mofimu kwa kutumia mfano mmoja wa sentensi kwa kila dhima.

5. "Kila sentensi ni tungo lakini si kila tungo ni sentensi." Fafanua usemi huu kwa kutumia mifano mitatu (3).

6. Njia za mwainisho wa ngeli zina udhaifu. Fafanua udhaifu wa mwainisho huo kwa kutoa mifano mitano (5).

## SEHEMU C (alama 20)

## MATUMIZI YA LUGHA

7. "Usanifishaji wa lugha huua sanaa." Jadili usemi huu kwa kutoa hoja madhubuti.

8. Lugha ya Kiswahili ina maneno yanayokuwa na maana zaidi ya moja. Eleza namna ya kuainisha tofauti hizo za maana kwa kutumia mifano mitano.

9. "Misimu ina tabia ambazo watumiaji wa lugha hawana budi kukubaliana nazo." Fafanua tabia hizo kwa kutumia mifano mitano (5) ya sentensi.



TATA PRINT-2007

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU D ( alama 20)

## UTUNGAJI

10. Jifanye wewe ni Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Kiandeni, S. L. P. 2010, Ikamba. Andika barua kwa Mkurugenzi wa Mitalaa, S.L.P 1020 Dar es Salaam ya kuomba kutumiwa orodha ya vitabu vipya vilivyopendekezwa kwa Fasihi ya Kiswahili vinavyotokana na Muhtasri mpya.

11. Andika insha ya maneno yasiyozidi mia nne (400) na yasiyopungua mia tatu (300) kuhusu Afrika na kombe la dunia mwaka 2010.

12. Jifanye wewe ni Afisa Elimu wa Wilaya ya Kinuka Mori uliyealikwa katika tafrija ya kumwaga Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mala aliyepewa wadhifa mwingine. Andaa hotuba utakayoitoa siku hiyo.

## SEHEMU E (alama 20)

## UFAHAMU

13. Soma habari hii kisha jibu maswali yanayofuata:

Najum alipopiga hodi nyumbani kwa Bwana Msa, Kikwajuni karibu na na Mnazi Mmoja, aliitikiwa na mtoto mdogo aliyekuwa akicheza mlangoni. Wakati ule Bwana Msa alikuwa msalani akioga, naye amekwisha kuagiza kuwa yeyote atakayekuja ana ruhusa ya kuingia ndani amngojee. Najum alikuwa kijana wa Kiarabu wa umri wa miaka ishirini na mitano, lakini nywele zake za kipilipili na pua yake alionesha waziwazi yeye ni **suriama**.

Najum karudi jana kutoka shamba yeye na Bwana Msa, baada ya **kukunjwa tanga** la Bwana Ali.

Sebuleni kwa Bwana Msa, alikoingia Najum hapakuonesha kuwa ni mahali pa kupumzika na kuzungumza. Viti vilikuwa viwili tu, kimoja kimesukumwa chini ya mvungu wa meza iliyokuwapo chini ya ukuta baina ya **mashubaka** mawili; cha pili kimekaa ovyo tu, katikati ya chumba. Hapana picha hata moja ukutani. Ila katikati ya ukuta wa mezani ilikuwepo saa nyeusi ya Japan imetundikwa kwa juu na chini yake ilikuwepo **rafu**. Pembeni pa mlango palikuwepo kabati la nguo kochini, akakivuta kiti kilichokuwepo chini ya meza, akakaa.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Najum alikiri kwamba elimu kama ile aliyo nayo Bwana Msa hakosi alipata katika kile kitabu chake, kiitwacho, Kinyume cha Mambo, kisichomtoka mfukoni na anachokisoma popote anapopata nafasi. Najum aliondoka juu ya kiti akakitafuta kitabu hicho tangu juu ya meza hata juu ya rafu, asikione. Basi alirudi kukaa kitako. Na hapo tena alipopapasa katika koti lililokuwa limevikwa juu ya mgongo wa kile kiti alichokalia, mara alirusha mkono wake kama mtu aliyeumwa na nge, na alipotazama kidole chake aliona kinatoa damu. Nini kilichomwuma vile? Aliondoka tena juu ya kiti, akachutama ili aone kilichomuuma. Kumbe ilikuwa sindano iliyopachikwa juu ya mfuko uliofumka nchani na umewahi kushonwa nusu. Najum kilimjia kicheko. Akacheka. Lakini kabla hajanyamaza kicheko chake, alisimama ghafula, akatumbua macho mlangoni kama mtu aliyepandwa na shetani au aliyeona jini. Kwa kweli hasa, Najum aliona mtu mweusi kama masizi amesimama mlangoni kimya akitazama nyendo zake, naye hana habari.

Kwa hakika, hakuna haja ya kufadhaika kwa namna ile kwa jambo lisilofadhaisha; lakini kwa dalili, sindano ilimpata vema hata asiweze kusikia mlio wa viatu vya miti. Bwana Msa alipokuwa anatoka kuoga akamkuta yeye anashughulika na koti lake. Lakini alipomjua kuwa ni yeye, kicheko chake kiliendelea kwa sauti kubwa. Juu ya meza, vitabu na karatasi vimetawanyika **mchafu koge**; lakini daftari moja lililokuwa wazi na kalamu juu yake, ilionesha kuwa Bwana Msa alikuwa akiandika kabla ya kwenda msalani kuoga. Najum alivyotuliza jicho lake juu ya daftari hiyo aliona maneno yaliyokuwa kwake ni **kichina**. Najum aliyasoma kirohoroho " Shibe Kamwamini njaa, na kwa hiyo akampa chakula amwekee." Najum akaendelea kusoma "Lakini Njaa alipomwona shibe kaondoka, alikichukua chakula chote akakiangamiza tumboni mwake."

Najum alikuwa tayari kumwamini kwa lolote atakalosema, ingawa alikubali kuwa ni vigumu wakati mwingine maneno yake kufahamika. Bwana Musa maneno yake makubwa anapotaka kumfahamisha mtu jinsi ubongo wake unavyofanya kazi, yalikuwa " Ukitaka kujua asili ya mwangaza ingia gizani au "Ukitaka kujua raha ya mtu aliyesoma, tazama tabu ya mtu asiyesoma."

**Maswali**

(a) Toa maana ya maneno yaliyokolezwa wino katika habari hii.

(b) Mwandishi anatoa ujumbe gani kwa hadhira yake?

(c) Eleza wasifu wa Bwana Msa na Najum katika habari uliyosoma.

(d) Mwandishi anaposema, " Shibe Kamwamini Njaa, na kwa hiyo akampa chakula amwekee, lakini Njaa alipomwona Shibe kaondoka, alikichukua



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

chakula chote akakisanganuza tumboni mwake." Unapata taswira gani katika usemi huo?

(e) Unafikiri ni sababu zipi zilizomfanya Najum kujiwa na kicheko wakati alipochomwa na sindano. Toa sababu mbili.

(f) Kwa maoni yako unafikiri ni kwanini Najum alihisi kuwa elimu aliyokuwa nayo Bwana Msa ilitokana na kusoma kitabu kiitwacho "Kinyume cha Mambo".

(g) "Ukitaka kujua asili ya mwanga ingia gizani" Usemi huu una maana gani? Methali gani ina maana sawa na usemi huu?



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org